



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
WIZARA YA AFYA
TAARIFA KWA UMMA**

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 28/04/2020.

Wizara ya Afya, Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya saba (7) wa Corona (COVID-19) nchini na kufikia idadi ya wagonjwa mia na tano (105) kutoka tisini na nane ambao tuliowatolea taarifa siku ya tarehe 24 Aprili 2020.

Wagonjwa wote wapya ni Raia wa Tanzania. Wagonjwa wote wametokea Unguja.

Jumla ya wagonjwa 36 wameruhusiwa kwenda nyumbani baada ya dalili zao za maradhi kuondoka ikiwemo homa, kikohozi, kifua kubana na kuumwa na kichwa. Wagonjwa wote hawa wameendelea kushauriwa kubaki katika nyumba zao kwa muda wa siku 14 na huku wataalamu wetu wa Afya wakiendelea kuwafuatilia kwa karibu kabla ya kuruhusiwa kurudi kwenye shughuli zao za kawaida za Maisha.


Serikali kupitia Wizara ya Afya, inaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji ya kutiririka na sabuni, kuepuka misongamano hasa katika huu mwezi mtukufu wa Ramadhani na kuhairisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima.

Aidha Wizara inaomba wananchi ambao wana dalili za homa kali, kukohowa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vyetu vya afya au kupiga simu namba 190. Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine na tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kueneza maambukizi na vifo vinavyo husiana na ugonjwa huu.

Pia vyombo vya habari vinahimizwa kupata taarifa za ugonjwa huu wa COVID-19 kutoka Wizara ya Afya.

Ndugu wananchi tuendeleo kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na kutuepusha na maradhi haya. AMIN.

Nawatakieni Ramadhan kareem


Hamad Rashid Mohamed (MBM, MBLW)

Waziri wa Afya -Zanzibar